

**MAELEZO YA HOJA ZILIZOSAINIWA NA KUONDOLEWA KWENYE  
ORODHA YA HOJA ZA MUUNGANO  
TAREHE 06 DESEMBA, 2022**

**1. Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi mara mbili**

**Hoja:** Kulikuwa na hoja kuhusu kuwepo kwa tofauti ya ukadiriaji wa viwango vya thamani za bidhaa, na kodi ya forodha baina ya Ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zilizoko Tanzania Bara na zile zilizoko Zanzibar kutokana na mifumo tofauti ya ukadiriaji. Tofauti hii ilisababisha kufanywa kwa makadirio mapya ya kodi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania Bara ambayo ni ya viwango vya juu. Hali hii ililetu malalamiko kwa wafanyabiashara wa Zanzibar, ambao nao walitumia kipengele cha Sheria ya Kodi kinachosema kwamba; "Bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kuitua kituo chochote rasmi cha forodha zihesabike kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania", na kwamba hakuna haja ya kufanya upya makadirio kwa bidhaa zinazoingizwa Tanzania Bara.

**Ufumbuzi:** Imebainika kwamba, wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa Zanzibar kutoka nje ya nchi na kupeleka Tanzania Bara hulazimika kulipia tofauti ya kodi iliyoachwa kukusanywa kutokana na tofauti ya tathmini ya bidhaa iliyofanywa Zanzibar. Hivyo, suala hilo haliwafanyi wafanyabiashara kulipa Kodi mara mbili badala yake kulipa kodi inayostahili kulipiwa kwa tathmini ya bidhaa inayotumika Tanzania Bara;

Hivyo, suala la ulipaji wa tofauti ya kodi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara linaelewaka vizuri kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

**2. Kodi ya Mapato - *Pay As You Earn (PAYE)* na Kodi ya Zuiro (*Withholding Tax*)**

**Hoja:** Kulikuwa na hoja kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hainufaiki ipasavyo na kodi ya mapato yatokanayo na mishahara ya wafanyakazi wa Taasisi za Muungano waliopo Zanzibar (PAYE) pamoja

na kodi ya kampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar (Withholding Tax).

**Ufumbuzi:** Kiasi cha shilingi **bilioni 1.75** kimekuwa kikitolewa kwa SMZ kila mwezi kuanzia mwaka 2012/13 ikiwa ni makubaliano ya muda yaliyopitishwa na kikao cha Baraza la Mawaziri wakati wa kujadili bajeti ya mwaka 2012/13. Imekubalika kuwa, PAYE kiasi cha shilingi **bilioni 1.75** kiendelee kutolewa kila mwezi kwa SMZ .

Kuhusu Kodi ya Zuio (Withholding Tax) kwa Kampuni zinazofanya kazi Tanzania Bara na zenye matawi Zanzibar, Wizara zinazohusika na Fedha za SJMT na SMZ mnamo mwezi wa Juni, 2022 zilikubaliana kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (**Tax Administration Act**) Sura ya 438, na Sheria ya Kodi ya Mapato (**Income Tax Act**) Sura ya 332 kupitia Sheria ya Fedha Nam.5 ya Mwaka 2022. Aidha, Mamlaka za Mapato za SJMT na SMZ zilitakiwa kuwa na makubalino (MOU) ya njia mwafaka ya kuwezesha Kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara na zenye matawi yake Zanzibar kuweza kulipa Kodi ya Zuio Zanzibar.

Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tayari imeshawasilisha marekebisho ya Sheria katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Makampuni Nam. 15 ya 2013, ili iweze kuendana na masharti mapya yaliyopo katika Sheria za Tanzania. Hatua hii itaondosha kasoro zilizokuwepo hapo kabla na itapelekea kuongeza ukusanyaji wa kodi ya makampuni kwa Zanzibar kwa makampuni yote yanayofanya shughuli zake Zanzibar ikiwemo Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*).

### **3. Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III)**

**Hoja:** Kulikuwa na hoja ya kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III) kutokana na Mkataba huo kuhusisha vifungu vya kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo.

**Ufumbuzi:** Baada ya SJMT na Benki ya Exim ya China kukubaliana na kuondoa kipengele kinachohusu kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo huo, SJMT ilisaini Mkataba wa Mkopo na Benki ya Exim China tarehe 03 Novemba, 2022.

#### **4. Ongezeko la gharama za umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO**

**Hoja:** Kulikuwa na hoja kwamba, mnamo mwezi Januari, 2008 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipandisha bei za umeme kwa wateja wa TANESCO ikiwemo Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme. Vilevile, mwaka 2011, bei za umeme pamoja na "Demand Charge" ziliongezeka tena, na hivyo kuibua malalamiko kwa watumiaji wa umeme kwa upande wa Zanzibar.

**Ufumbuzi:** Menejimenti ya ZECO na TANESCO zilikutana tarehe 15 Novemba, 2021 kujadili taarifa iliyoandaliwa na wataalamu wa Mashirika yote mawili. Katika kikao hicho suala la bei ya kuuziana umeme kati ya TANESCO na ZECO lilipatiwa ufumbuzi ambapo Wajumbe walikubaliana ZECO kununua umeme kwa shilingi 130 kwa uniti moja kama ilivyopendekezwa na ZECO.